# Maoni juu ya makala ya S.M. Sanka "Dhana za Umapokeo na Usasa katika Ushairi wa Kiswahili"

M.M. Mulokozi

1. Mwandishi anajadili dhana za "umapokeo" na "usasa" kama zinavyojitokeza katika mijadala kuhusu ushairi iliyopamba moto kuanzia miaka ya 1970. Anazitazama dhana hizo katika muktadha mpana wa vuguvugu la "modernism" la Ulaya na Marekani la mwanzoni mwa karne hii. Anakataa mtazamo unaohusisha mgogoro huo na "umbo" tu, na anaelekea kupendekeza kuwa "usasa" ufungamanishwe na maudhui na muktadha wa kihistoria.

2. Mtazamo wa mwandishi ni mpya, kwa maana ya kuwa ni tofauti na mitazamo ya wahakiki wengine waliozungumzia suala hili. Hivyo, ni mchango mzuri katika kuendeleza mjadala kuhusu ushairi wa Kiswahili.

3. Mambo yafuatayo yanahitaji kujadiliwa zaidi:

3.1 Dai la kuwa wahakiki waliuainisha ushairi wa Kiswahili katika makundi makuu mawili (yaani "ya kimapokeo" na "ya kisasa") lahitaji uthibitisho zaidi. Marejeo yanayohusika pia yatajwe. Nikumbukavyo mimi, wakati wa mjadala zilitumika dhana nyingi. Baadhi yake ni "ushairi wa kimapinduzi", "ushairi-huru", "mavue", na "tungo-mtiririko". Wahakiki walikuwa katika matapo kadha. Baadhi walidai kuwa "tungo-huru" si mashairi. Kwa kundi hilo, ushairi wa Kiswahili ulikuwa katika fungu moja tu la "ushairi wa mapokeo". Kwa mfano, Mayoka (1984: 34-35) hakubali kuwa tungo za Kezilahabi ni ushairi au sanaa. Amri Abedi (1954: 16) aliugawa ushairi katika mafungu ya mshairi yenye kufuata kanuni za vina na mizani na mashairi "guni" - yasiyofuata kanuni hizo. Dhana ya "usasa" ilijitokeza hasa baada ya kuchapishwa kwa diwani ya *Mashairi ya Kisasa* (K.K. Kahigi na M.M. Mulokozi). Diwani hiyo ilitoka hadharani mwaka 1975, japo tarehe rasmi ya kuchapishwa ni 1973. Jina la diwani hiyo halikukusudiwa kuelezea umbo, bali lilikusudiwa kuelezea maudhui na wakati: watunzi walitaka kusisitiza kuwa walikuwa wakijadili matatizo ya wakati wao, yaani <u>sasa</u>.

3.2 Kama tukiainisha "umapokeo" na "usasa" kwa mujibu wa mawazo, itakuwa vigumu kuamua kuwa "usasa" unaanza mwaka 1970 kama mwandishi anavyopendekeza. Ni kigezo kipi kinatumika kuamua kuwa maudhui fulani ni "ya kisasa"? Mbona mashairi yenye mawazo ya kutetea wanyonge kama yale ya S.A. Mohamed yalikuwa yakitungwa hata kabla ya mwaka 1970? Kadhalika, iwapo "usasa" utahusu fani, vile vile itabidi turudi nyuma zaidi, maana tungo zinazokiuka kanuni za urari wa vina na mizani zimekuwepo wakati wote (tangu enzi za Liyongo), japo zimepata nguvu zaidi kuanzia miaka ya 1960. Mfano mzuri ni tafsiri za Shakespeare zilizofanywa na Nyerere, na ambazo zilizua mjadala kati ya Amri Abedi na Lyndon Harries (angalia "Utangulizi" wa Amri Abedi katika diwani ya Mnyampala ya Waadhi wa Ushairi (1965)).

3.3 Ninavyokumbuka mimi mjadala mkubwa ulihusu umbo la ushairi, haukuhusu maudhui hasa. Washairi wa pande zote mbili walikubaliana katika masuala mengi isipokuwa lile la kudai kuwa vina na mizani ndio "uti wa mgongo" au kigezo kikuu cha ushairi wa Kiswahili. Iwapo "usasa" utahusu maudhui, basi itabidi mjadala mzima ubadilike. Maana ingawa "wanausasa" wengi ni

waasi kifani na kimaudhui, lakini haiwezekani kuwaweka wote katika tapo moja la fikira au falsafa; wanatofautiana sana. Aidha, wanajadi vilevile wanatofautiana sana kifikira.

3.4 Chiraghdin hakudai kuwa "ulinganifu wa vina na mizani ndiyo kitambulisho pekee cha ushairi wa Kiswahili." Hata sehemu iliyodondolewa haisemi hivyo. Itazamwe kwa makini zaidi. Sifa ya la lugha teule vilevile anaitambua.